

Ngurumo Saba za Ufunuo 10

Ufunuo 10:1-11

“Kisha nikaona Malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni. Amevikwa wingu; na upinde wa mvua juu ya kichwa chake; na uso wake ulikuwa kama jua, na miguu yake kama nguzo za moto. Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa. Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi. Naye akalia kwa sauti kuu. Kama simba angurumavyo. Na alipolia, zile ngurumo saba zikatoa sauti zao. Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao nalikuwa tayari kuandika. Nami nalisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo Ngurumo saba, usiyaandike. Na yule Malaika niliyemwona, akisimama juu ya bahari na juu ya Nchi, akainua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni, akaapa kwa Yeye aliye hai hata milele na milele, Yeye aliyeziumba mbingu na vitu vilivyomo na Nchi na viti vilivyomo. Na bahari na vitu vilivyomo, ya kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya: Isipokuwa katika sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa; kama ilivyo wahubiri watumishi wake Manabii.....”

Acha tusikie kile Nabii wa Mungu alichosema, ametuhimiza kwa maneno yafuatayo:

Hebu chukuwa yoyote ya mabatizo haya ya uongo; fulani na fulani na fulani za uongo. Sijali linavyo sikika kuwa halisi, jinsi wanavyojaribu kuiga, ni uongo kama ni kinyume cha Neno la Mungu la wakati huu. Hivyo ni kweli hasa. Unasema. Vema, vema, tulifanya jambo hili. na tunafanya jambo hili, na kanisa letu ni namna hii na namna hii na namna ile” sijali ni nini. Kama ni kinyume cha Neno lililo andikwa la wakati huu, ni uongo. Mungu hatakuwa na uhusiano wowote nalo, haidhuru ni aminifu namna gani, ni la kielimu jinsi gani, ni la kiakili jinsi gani, linasikika la kweli jinsi gani, Iwapo ni kinyume cha Neno la Mungu la wakati huu.....

Sasa ili kusoma andiko kwa makini, Paulo alimwambia Timotheo. Yasome kwa usahihi ukiligawanya Neno la Mungu ambalo ni kweli”.

Ndipo sasa kuna lazima tatu katika maandiko. Katika kutumia Neno la Mungu kuna mambo matatu ambayo hupaswi kufanya. Sasa hupaswi kulitafsiri Neno vibaya. Unasema . “vema, naamini hivi, linamaanisha kile tu lisemacho halihitaji mtafsiri. Na lazima usiweke Neno mahali pasipo pake.

Na hupaswi kuondoa Neno sehemu yake. Na tukifanya moja ya haya, Itaitupa Biblia nzima katika kuchanganyikiwa na machafuko.

Sasa sikiliza: Lakini kumbukeni, Daniel aliambiwa na yule Malaika. Danieli alisikia zile ngurumo saba zilitoa sauti zao. Danieli akanyakuwa kalamu yake akaanza kuandika, ndipo Malaika akasema, usiandike hilo” Amina (Danieli 12:4,9). Je mko tayari?

Hebu tuingilie jambo hili dakika hizi kwa dakika tano zinazofuata sivyo? Sikilizeni, usiandike!” Yohana aliona jambo lile lile, na tayari lilikuwa limeandikwa upande wa nje wa Biblia; na kulikuwa na muhuri saba nyuma ya kile kitabu, ambapo hapana mtu angaliweza kuzifungua muhuri hizo, hizo zilikuwa sauti. Hii hapa Biblia, imeandikwa, ambayo ni siri, yenyewe. Basi upande wa nyuma wa Biblia, zile funuo kama zilivyoonyeshwa Daniel, zinasema kuna sauti saba zitakazo nena, ambapo hapana mtu angaliweza kuzifunua, hakuna mtu anayejua zilikuwa ni nini, bali Biblia ilisema na Danieli na Yohana waliambiwa ya kwamba “katika siku za mwisho, sauti hizi saba zingejulikana na kanisa la kweli”. Mnalipata jambo hilo? Unaweza kuona mahali ambapo ule uongo na kuigiza kunajaribu kuweza kuwaweka watu mashuhuri mbali na mahali hapo?

Sasa mjumbe huyu wa Malaki 4:5-6 na Ufunuo 10:7 atafanya mambo mawili. Moja kulingana na Malaki 4 ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao. Pili atafunua siri za ngurumo saba katika ufunuo 10 ambayo ni mafunuo yale yaliyo ndani ya zile mihuri saba. Hizi “kweli za kisiri zilizo funuliwa kiungu ndizo zitakazo igeuza kweli mioyo ya watoto iwaelekee baba zao wa kipentecoste ndio hivyo kabisa.

Sawa hapa kulikuwa na “sauti”. Oh, jinsi tunavyozihitaji hapa Jeffersonville maelfu ya sauti zilizo hai, Ngurumo ya Mungu zikinguruma katika hali ya utamu, na katika utukufu, usafi, maisha yasiyo chafuliwa. Wakitembea ulimwenguni leo bila ya kuwa na lawama. Ndio Bwana, wakristo halisi, hiyo ni ngurumo dhidi ya adui. Shetani hajali jinsi gani unaweza kuruka, jinsi gani unaweza kufanya hivi au kupiga kelele. Bali kile kinachomdhuru shetani ni kuona kule kutakaswa, maisha matakafu yaliyowekwa wakfu kwa Mungu; mnene chochote kile, mwite chochote.

Mtamu vile awezavyo kuwa na kuendelea. Oh jamani.Hilo humtupa mbali;hiyo ndiyo ngurumo ambayo inamtingisha shetani.

Na hiki kitabu kilichogawanywa mara saba chenye mipango saba ya ukombozi kimeletwa kwetu na hicho ndicho kile kitabu kimeshikilia. Sasa tuangalie hapa katika sura ya 10 ambapo huyu Malaika mkuu ametangaza jambo fulani. Na alikuwa na kitabu kidogo ambacho Yohana alipaswa kukila na alipoanza kukila kilipofika tumboni mwake kilikuwa kichungu. Lakini mdomoni kilikuwa kitamu (Ufunuo.10:8-11).

Na wakati kilipoingia tumboni kisha kinakuwa kichungu. Kila mtu anakuwa kinyume na wewe, kila mtu anakuambia “mtakatifu wa kujifingirisha, u hiki vile ama vinginevyo.Unaona. umerukwa na akili.”Hivyo ni vigumu kukielewa. Bali unaposhuhudia utukufu wake, ni kitamu mdomoni mwako. Hilo tu. Unaona? Na usimamapo mkutanoni, unasema, “utukufu kwa Mungu. Alelu.....”Ee, na unapopitia hilo pingamizi kubwa ni vigumu, bali ndiposa unapotoka katika hilo pingamizi kuu.Unaweza ukalitolea ushuhuda. Ndipo sasa ni kitamu mdomoni.Unaona? Hiyo ni kweli, hicho ndicho kitabu cha ukombozi.

Wa saba na wa mwisho ya hii mihuri, wakati ilipokuwa ikifunguliwa, inapatikana katika Ufunuo sura ya10, kulikuwa na Malaika mkuu (ambaye alikuwa ni Kristo) akishuka na kuweka mguu mmoja nchi kavu na mmoja baharini,na kuinua mikono yake juu,na kusema, “siku zimekwisha. Wakati unatoweka.Yote yamekwisha.Hakutakuwa na wakati tena”.Na Yeye akasema katika kule kutoa sauti ya.....Katika wakati huu siri za Mungu zitamalizwa.Mungu ni nani, na jinsi gani alivyojidhihirisha; na jinsi mihuri ilivyofunuliwa, jinsi tunavyoanza sasa na jinsi alivyokuwa Mwana wa Mungu.Alikuwa Mungu Yeye mwenyewe aliyefanyika mwili.Na ufunuo wa kile Yeye alichokuwa; hilo lingepasa limalizike kabla huyu Malaika hajaweza kuweka miguuyake juu ya nchi na baharini, na kuapa kwamba hakutakuwa wakati tena, wakati nyakati hizo zitakapokuja.Tuko hapa katika uwanja wa mbele wa jambo hilo sasa.Wa mwisho wao ni Ufunuo 10, mguu juu ya nchi na juu ya bahari, muda umekwisha, ukombozi umemalizika; sasa Yeye anakuja kama Simba.Yeye alikuwa Mwana Kondoo awali; sasa Yeye anakuja kama simba wa kabila wa Yuda

Ingewezekana kwamba ile ngurumo kuu au Yule malaika wa saba, katika lile kundi la wale saba kundi la kipindi cha saba, piramidi iliyoundwa katika umbo, watatu kila upande,na moja juu,nao walishuka toka umilele. Je! yawezekana Ni siri ya ngurumo ambayo itarudisha lile jiwe kuu la

kuwekwa juu? Unajua, ile piramidi haikutiwa kamwe kifuniko.Lile jiwe la kuwekwa juu halijaja bado. Limekataliwa.Ndivyo ilivyo,Ndugu,Dada.

Kile ambacho tumeona kinatokea kingepaswa kuweka kila nafsi katika kitendo.Kingepaswa kulifanya kanisa ambalo wangelifanya uamsho hapa Phoenix. Kwamba watu wangeliruka kwa ndege kutoka Ulaya kuona kile kilichotokea.Wangelipaswa kusema kuna mahali huku Arizona paitwapo bonde la Maricopa, Mji uitwao Phoenix.Kuna jambo fulani limetendeka pale mpaka ngurumo 7 za Ufunuo 10, ambazo hata hazikuandikwa katika Biblia.Zimekuwa zikidhihirishwa.”

Tuko kwenye mafundisho, na unaweza ukatambua hangaiko kubwa la akili lilivyo juu yangu; kwa sababu kama nikifundisha chochote cha makosa, nitakwenda kujibu kwa hilo. Unaona? Na kwa hiyo silazimiki kuchukuwa asemacho yeyote. Lazima liwe limevuviwa.Na naamini kwamba Malaika saba wanaoshikilia hizi Ngurumo saba wataridhia hili.

Hiki kitabu cha mihuri saba kinafunuliwa kwenye wakati wa zile Ngurumo saba za Ufunuo 10. Sasa, ile siri ya hiki kitabu cha mihuri saba kinafunuliwa kwenye kupigwa baragumu, kwa ule ujumbe wa malaika wa kanisa la saba unaona? Malaika wa saba atakakapoanza kupiga baragumu na pale ni jumbe zimeandikwa kule,Nasi tunazo katika umbo la kanda na vitabu. Sasa, lakini ni kitabu, kitabu cha kimafumbo. Ni kitabu cha ukombozi, Na sasa tunajua kuwa hiki kitabu cha ukombozi hakitaeleweka vizuri.Kimechunguzwa kwenye kupitia vipindi sita vya kanisa.Lakini mwishoni wakati wa yule Malaika wa saba anapoanza kupiga baragumu fumbo lake, atamaliza mambo yote yenye miisho iliyo achia ambayo hawa watu waliichunguza.Na zile siri zinashuka kutoka kwa Mungu.Kama Neno la Mungu na linafunua ufunuo mkuu wa Mungu. Ndipo Uungu na kila kitu kinawekwa sawa. Siri zote; uzao wa nyoka na mengine yote yatafunuliwa.

Sasa,unaona,silifanyi tu hilo.Hilo ndilo HIVI ASEMA BWANA.Nitawasomea toka kwenye kitabu; “kupiga baragumu kwa ujumbe wa Malaika wa saba, ile siri yote ya Mungu imekwisha, lile lililonenwa na Manabii wake watakatifu yaani wale Manabii walioandika Neno, wakati wa kupiga baragumu wakati wa saba wa mwisho wa kanisa, sehemu zote zilizoachwa zitakusanywa pamoja, na mihuri inapovunjwa na siri zimewekwa wazi, Malaika anashuka, mjumbe Kristo anaweka mguu wake juu ya nchi na juu ya Bahari, akiwa na upinde wa mvua juu ya kichwa chake. Sasa kumbuka, huyu Malaika wa saba yuko duniani kwenye wakati wa kuja huku.

Na mwishoni mwa kipindi cha pentecoste tunatakiwa kupokea,kufuatana na Neno, kama Mungu atakavyonisaidia usiku huu kuwaonyesha kupitia hapa, kwamba tunapokea mjumbe yule atakayechukuwa miisho yote iliyoachiwa huko kote na kufunua siri yote ya Mungu kwa ajili ya kunyakuliwa kwa kanisa.

Na ndipo zinakuja ngurumo saba za siri ambazo hata hazijawahi kuandikwa kabisa. Hiyo ni sahihi. Na naamini kwamba kupitia Ngurumo zile saba zitafunuliwa katika siku za mwisho ili kumkusanya bibi arusi kwa imani ya unyakuo,kwa sababu tulichonacho sasa hivi, tusingeweza kulifanya hilo.kuna jambo fulani tunatakiwa kusonga mbele. Sisi imetuwia vigumu kuwa na imani ya kutosha kuponywa na kubadilishwa. Kufumba na kufumbua na kunyakuliwa juu kutoka katika dunia hii. Na tutalipata hilo baada ya muda kidogo. Bwana akipenda,tutapata lilipo andikwa.

Kwa hiyo Yohana anakwenda kutazama/kuangalia kilikuwa kitu gani.Yohana anakwenda kuona kile Ngurumo ilichosema. Ndio wakati kiumbe huyu alipomwambia Yohana. Njoo uone siri iliyokuwa chini ya muhuri wa kwanza.Ile ngurumo, ile sauti ya muumbaji imenena hilo.Sasa alipaswa kujua kilichokuwa pale, Amina.Oh jamani,Lakini fikirini sasa aliandika hili.Lakini alipoanza kuandika zile nyingine ngurumo saba.Yeye alisema, “ Usiyaandike”Alikuwa ameagizwa kuandika kila kitu alichokiona.Lakini hizi ngurumo saba katika ufunuo 10 ziliposema,toa sauti Yeye alisema, usiyaandike hata kidogo’.Ni siri.Bado hatujui hizo ni nini;lakini oni langu zitafunuliwa moja kwa moja.Na zitakapofunuliwa zitatoa imani kwa ajili ya ile neema ya unyakuo ili lile kanisa liondoke. Tumepita tu kila kitu tunachojua; katika majira yote tumetazama kila kitu. Tumeona siri ya Mungu. Tumeona kule kukusanyika kwa Bibi- Arusi katika siku za Mwisho. Lakini bado kitu pale ambacho hatuwezi kujiangaza nacho wenyewe. Kuna kitu kingine. Lakini ninawazia wakati zile siri zitakapoanza kujitokeza....Mungu alisema, “subiri sasa.Ngoja kidogo.Nitazifunua siku ile. Usiziandike hata kidogo.Nitazifunua siku ile.Usiziandike hata kidogo, Yohana kwa sababu watakwazika juu yake liache hilo.Lakini nitazifunua siku ile itakapohitajika kufanyika”.

Ngurumo saba za ufunuo....yeye atamuonyesha Bibi Arusi jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya Imani kuu ya kubadilishwa. Sasa, acha tuone mifano. Tunaona nini Ngurumo ilimaanisha. Hilo ni kamilifu; tunajua hilo? Unaona? Ngurumo ilikuwa ni sauti ya Mungu wakati muhuri ulipo funuliwa.

Tunataka kupokea neema ya kunyakuliwa. Tunataka tuweze, wakati ile ngurumo ya siri itakapo nguruma pale na Kanisa linachukuliwa juu, tunataka kuwa tayari kuipokea. Bwana tujalie.

Bibi Arusi bado hajawa na uamsho. Hakuajawa na uamsho pale. Hakuna udhihirisho wa Mungu wa kumtikisa Bibi Arusi bado. Unaona? Tunalitazamia sasa. Itahitaji zile ngurumo saba zisizojulikana nyuma kule kumwamsha tena. Yeye atatuma, aliahidi hilo. Sasa, angalia yeye Bibi Arusi alikuwa amekufa.

Sasa mlango wa 8 linafunua tu tukio la muhuri wa saba ambapo hakuna kitu kingine kinachofunuliwa. Sasa, hii haina uhusiano wowote na mlango wa 7 wa ufunuo. Ni kufunuliwa kwa Muhuri wa saba ambapo ni kwa ukimya. Na kama ningekuwa na muda tu, (nitajaribu sehemu fulani) kuwaonyesha, ukirejea nyuma kote kuanzia kitabu cha mwanzo huu sura ya saba... huu muhuri wa saba unazungumziwa. Kuanzia pale nyuma katika kitabu cha mwanzo, huu wa saba... Mihuri hii kuanzia chini hadi juu.

Ile namba kamilifu. Ngurumo saba zikifuatana, zilitoa sauti zao sio kama tu moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, ilikuwa(Mfululizo) moja kwa moja. Ndipo Mbingu hazikuweza kuandika hilo. Mbingu haziwezi kafahamu kuhusu hilo, wala kingine chochote, kwasababu hakuna jambo lililoendelea. Lilikuwa ni wakati wa mapumziko. Lilikuwa kuu mno hata malaika walifichwa.

Sasa,sasa, umetazama katika kufunuliwa kwa muhuri wa saba, iko pia katika fumbo lenye awamu tatu. Hii moja ninayo..... itazungumza na nimekwisha zungumza, hilo ni fumbo la zile ngurumo saba zile ngurumo saba kule Mbinguni zitafunua fumbo hili la zile ngurumo saba. Itakuwa ni wakati wa kuja kwa Kristo, kwasababu Kristo alisema hakuna hata mmoja aliye jua ni lini angerudi.Je uliona wakati wayahudi walipo muuliza Yeye hilo? Unajua tunapolinganisha lile andiko hapa mathayo 24, na Mihuri sita, ule Muhuri wa saba uliachwa; kwa sababu Kristo alisema ni Mungu tu mwenyewe ajuaye, wala hata malaika hawajui, si ajabu, wala hata haikuandikwa. Unaona, walinyamaa; Hakuna lililotendeka wakati huo. Malaika hawajui hilo. Hakuna mtu anayejua ni lini Yeye anakuja. Lakini kutakuwepo na kutakuwepo na sauti saba za hizo ngurumo ambazo zitafunua huo ufunuo mkuu kwa wakati huo. Kwa hiyo ninaamini, kwetu sisi ambao... kama hatujui hilo, na kama tuki... Haliwezi kujulikana mpaka wakati huo, lakini itafunuliwa katika

siku ile katika saa ambayo hilo linapaswa kufunuliwa. Kwa hiyo jambo ninalopaswa kufanya ni sisi kuwa wanyoofu mbele za Mungu na kumtumikia Yeye na kufanya yote ambayo tunajua jinsi ya kufanya, na kuishi maisha mema na ya Kikristo. Hapa, sasa, tunakuta ule muhuri wa sita umekwisha kufunguliwa kwetu, tunaona, na tunajua kuwa huu muhuri wa saba hauwezi kuvunjwa na kutangazwa kwa watu mpaka ile saa ifike. Sasa kuna sababu fulani kuwa Mungu aliruhusu hizi sauti saba zingurume. Kwa sababu ni lazima ije. Kwani ile..... Tunakuta Kristo aliye Mwana-Kondoo achukua kile kitabu mkononi mwake, na alifungua ule muhuri wa saba. Lakini unaona ni siri iliyofichwa. Hakuna ajuaye, bali inafuatana moja kwa moja na lile Yeye alilosema: Hakuna hata mmoja angejua kuja kwake, wao pia wasingejua kuhusu hili fumbo la Ngurumo saba. Kwa hiyo unaona imeunganishwa pamoja. Leo tumekwisha pata ufahamu kiasi hicho kuhusu hili, kwa sababu yote yaliyo salia tayari yamekwisha kufunuliwa, bali hilo bado halijafunuliwa. Lakini wakati nilipokuwa nimeketi chumbani kwangu na nikisikia hili au siyo kusikia, samahani lakini niliona likifunuliwa ikawa ni hizo Ngurumo saba: sasa, hicho ndicho kiasi tutakachoweza kufikia hapo hapo. Na sasa natumaini kila mmoja wenu atamtumikia Mungu na kufanya kile ambacho ni sahihi, na umpende maisha yako yote na kumtumikia Yeye na Mungu atayashughulikia yote yaliyo salia. Sasa tunayo katika kumalizia hapa sasa kwa neema ya Mungu siri zote za ile Mihuri sita ambao zilikuwa zimefungwa na Muhuri, na tunaielewa na kujua hapa kuwa ule muhuri wa saba haupaswi kujulikana kwa Umma. Sasa, kurudi kwake, na penye saa ya kurudi kwake, wakati wa maangamizi ya Dunia..... unajua, Yeye alisema hapa, ni nini itakuwa Ishara ya kurudi kwako na ya mwisho wa dunia/ katika Mathayo 24. ndipo hapa walipomuuliza Yeye hilo swali, Yeye aliingia kwa undani swali hilo. Alieleza kuhusu Israeli kukusanyika kama Taifa katika Aya ya 31 ya Mathayo 24:31. lakini ndipo aliachia na kuingia kwenye mithali. Unaona? Ndipo unaona ile, “Jifunzeni mfano wa mtini, Tawi lake likiisha kuchipua na kuchanua majani, kwa nini, mwatambua kuwa wakati wa mavuno u karibu”. Na ndipo “myaonapo haya yote tambueni ya kuwa wakati wa mavuno u karibu”. Na ndipo myaonapo hayo yote tambueni ya kuwa yu karibu mlangoni. Unaona Israeli wakikusanyika katika nchi yao wenyewe. Lakini ukitazama , Ameuwacha ufunuo huu wa muhuri wa saba. Na wakati ule muhuri wa saba, wakati Yeye alipoufungua, ameuacha tena. Unaona? Hivyo tunaona kuwa hiyo ni siri kamilifu, hivyo basi saa haijatimia bado kwa fumbo hilo kujulikana. Hivyo basi, tupo umbali huu na sehemu iliyosalia itajulikana wakati utakapo wadia wa Yesu kuja duniani tena kwa ajili ya Bibi Arusi wake, au chochote kitakachotokea wakati huo. Sasa hadi wakati huo, hebu sote tuwe tunaomba tuishi maisha ya Kikristo. Mema yaliyonyoka, huku

tukitazamia kuja kwake. Na sasa kanda hii ikitokea kuangukia mikononi mwa watu mahali fulani usijaribu kufanya isimamishe msimamo wa “kimafundisho”. Jambo la kufanya tu ni kuendelea kumwishia Mungu. Kwa sababu hii siri kuu ni kuu mno hata Mungu hakumruhusu Yohana aiandike. Ilinguruma, lakini Yeye alituahidi kuwa ingefunuliwa, lakini hadi wakati huu. Haijafunuliwa. Sasa Mungu alikuwa na kusudi na siri iliyofichika. Na hilo ndilo nataka kuongea juu yake kwa Kanisa asubuhi hii, ile siri ya Mungu ilifichika, ile Yeye aliyokuwa nayo katika nia yake kabla dunia haijaanza na jinsi inavyojifunua yenyewe moja kwa moja mpaka wakati huu wa sasa ambao tunaishi. Ndipo mtaelewa kwa ufasaha basi, kile kilicho fanyika. Siri kuu ya Mungu ya jinsi...lilivyo fumbo. Aliiweka kuwa fumbo hakuna mtu aliyejua chochote juu yake; Hata Malaika hawakuelewa. Unaona? Yeye hakufunua. Hivyo ndiyo sababu, chini ya siri yetu ya saba. Wakati ule muhuri wa saba unapofunuliwa kulikuwa na ukimya. Yesu alipokuja duniani. Walitaka kujua Yeye angerudi tena lini. Yeye alisema, “Siyo.....Hata Mwana mwenyewe hajui ni wakati gani itatokea”. Unaona, Mungu alikuwa na lote hili Yeye mwenyewe ni siri. Na hiyo ndiyo sababu kulikuwa na ukimya mbinguni muda wa nusu saa. Na ngurumo saba zikatoa sauti zao, naye Yohana alikatazwa kuandika....kule kuja kwa Bwana. Hilo ni jambo moja ambalo halijafunuliwa bado, juu ya jinsi Yeye atakavyo kuja. Na lini atakuja Ni jambo jema kwamba Yeye hafanyi hivyo. Hapana Yeye amelionyesha au kulifunua katika kivuli kwenye Biblia. Kwa hiyo, Biblia nzima ni Ufunuo wa siri ya Mungu katika Kristo. Lo, Biblia nzima ni onyesho la nia moja aliyokuwa nayo Mungu kusudi moja alilotaka kulitimiza katika Biblia yote. Na matendo yote ya waamini katika Biblia yalikuwa ni kwa ulinganisho kuelezea. ile nia ya Mungu ni nini. Na sasa katika siku hii ya mwisho Yeye amelifunua na kulionyesha. Na kwa msaada wa Mungu, mtaliona hapa hapa asubuhi hii: Kile Bwana alichokuwa nacho katika nia yake wakati wote amekionyesha kwa hiyo basi unaweza kuona maana kuu ya kile kilichokuwa ili kulijua hili na ndipo unajaribu kulileta kwa watu. Unaona? Na ninyi hamfanyi.....sijaingia ndani kujaribu kueleza kama Mungu alivyolifunua kwangu.

Sasa, kule kuja kwa Bwana ni siri. Hatujui yeye anakuja lini, anakuja namna gani, lakini tunajua anakuja, unaona? Na kwa hiyo ndivyo siri zote zinavyosubiri hii siku ya mwisho. Baada ya Yeye kumaliza ndipo amefunua, na kuonyesha kile alichofanya Lo. Jamani. Hakuwahi kutoa siri yake yote kwa ukamilifu.

Ni kama hii tu, kulinganisha mihuri saba sasa, Mungu alipomtumia Martin Luther kwa kutoa kwa lile kanisa la kwanza (kile kipindi cha kanisa) na alipomtumia John Wesley, na kwa pole pole aliwaleta nje na alikuwa akifunua kwao kile kipindi cha kanisa wakati sisi....Yoyote anaporejea katika Biblia sasa na kugundua lakini katika siku za mwisho.

Sababu likawa jambo kuu hivi kwamba alisema juu yake hapa na kuonyesha zile Ngurumo saba. Na magazeti ya “Cook” na “Life” Gazeti la Life, lilionyesha ile duara ya wingu na nuru pale ambavyo wasingeelewa na bado hawajui, lakini hapa akisema” Nenda kule na usubiri kufunuliwa kwa hizi Siri” na kwa miezi hapa kabla haijatokea: na ndipo ikatokea, kwa usahihi tu jinsi Yeye alivyosema ingekuwa.

Mliona katika ile picha hata yule Malaika upande wa kulia alipokuwa akitokea akishuka na mabawa yake nyuma na kichwa chake kimekaa pembeni? Iko moja kwa moja pale katika ile picha kwa usahihi tu. Kwa miezi kabla haijatokea niliwaambia hapa kuwa , Yeye anakwenda kuleta mwili wa waamini pamoja, kufunua, mambo yaliyopotoshwa. Kila mmoja, wamekuwa wakinijia kila wakati wakisema ndugu Braniham zile ngurumo saba ambazo zilitoa sauti zao na Yeye akasema “Usiandike lakini ya funge” wakasema je hizo, zitakuwa ni zile ngurumo saba zitakazofunuliwa katika siku za mwisho? Unaona, ngurumo saba ambazo zitatuambia? Sasa hiyo haionekani ni kitu kizuri sana? Unaona? Lakini uwe macho kuwa unasema juu ya nini unaposema hilo. Yeye alisema hakikisha kuwa huyaandiki hayo. Hizi ngurumo saba zilitoa sauti zao, na Yeye akasema “usiandike hilo, lakini inapasa ifungwe kwa muhuri katika kitabu hadi siku ya mwisho”.

Sasa,mtu mmoja amekuwa, wengi wamekuwa wakiniambia na wanathiolojia wamekuwa wakisema ndugu Branham kama Bwana Mungu..... wakisema, kwamba pamoja na ujuzi ulionao ambao Bwana amekupa kwa ajili ya watu wake, wakisema hivi kwa unyenyekevu, wakasema mwenyewe sasa, hakuna chochote ambacho hakijafunuliwa katika muhuri wa saba, Neno lako lile ambalo limedhihirishwa. Nilisema hilo lingeweza kuwa kweli. Unaona, na nikasema “lakini unaona siwezi kufanya hilo” Yeye alisema kwa nini huwezi kufanya hilo? Unazo sifa zote. “Nikasema” Basi utazame, Neno moja haliwezi kuongezwa au kuondolewa. Unaona? Na akasema vema basi hizo ngurumo saba unajua? Akasema. “Je zile ngurumo saba zinaponguruma haiwezekani kuwa ni ufunuo ambao mtu fulani atapewa? “Nikasema hapana Bwana hiyo ingekuwa ni kuongeza kitu fulani kwa hilo au kuondoa kitu fulani kutoka hilo”, yote yamefunuliwa pale. Na ni zile mihuri saba ndiyo iliyo funua

ufunuo wa hizo kuwa zilikuwa nini? Yeye bado ndiye Neno unaona hawezi kutoka nje ya lile Neno haiwezi ikaacha Neno. Na Roho wa Mungu hawezi kuliacha lile Neno. Yeye atakaa moja kwa moja na lile Neno akiwapofusha baadhi na kufumbua macho ya wengine siku zote Yeye atafanya hivyo.

“Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa zinazosomwa na watu wote”. Au, “ninyi ni.”.. Tafsiri hilo, geuza kuzunguka hivi, unaona. Ugeuze tu lote, Ninyi ni nyaraka ambazo zimekwisha andikwa, kwani huwezi kuongeza chochote kwa hilo. “hizo zinasomwa na watu wote”. Neno la Mungu lililodhihirishwa, kwa maneno mengine.

Na petro na Yohana, ili kulionyesha hilo, wakati walipokwenda juu pale. Watu walielewa kuwa wao walikuwa ni watu wajinga na wasio na elimu. Lakini walizingatia kuwa walikuwa na Yesu unaona? Walikuwa wajinga na wasio na elimu lakini walikuwa nyaraka zilizoandikwa, zilizoandikwa kwamba wao walikuwa na Yesu. Kwa sababu Yesu alikuwa anajidhihirisha mwenyewe kupitia wao. Kristo alikuwa amefunikwa na pazia katika miili yao, aliyedhihirishwa, amekuwa hai, kama alivyokuwa ndani ya Musa.

Angalia nataka kusema jambo moja zaidi kwa makini sasa; msikose jambo hili.Jinsi linavyoshangaza. Kutoka kwa Ujumbe wa Malaika wa saba (yule mjumbe wa ule Muhuri wa Saba). (na Ufunuo10 ilikuwa Muhuri ya Saba) mpaka kwenye Baragumu Saba katikati ya nyakati hizo mbili ... Sasa, mara Kanisa hili Bibi Arusi linapovutwa pamoja, linanyakuliwa ndani ya ile siri ya Muhuri ya Saba, ama Muhuri ya Saba, siri ya kwenda. Nao wayahudi wanaitwa kwa siri ya Baragumu ya Saba ambayo ni manabii wawili Elia na Musa.

Je zile ngurumo saba ambazo ni sawa na zile siri saba zimekwisha kufunguliwa? Je, zilifunuliwa katika zile Muhuri saba, ila bado hazijajulikana kwetu kama ngurumo bado?

La, zilifunuliwa katika zile muhuri saba; hivyo ndivyo zile ngurumo zilicho kuwa zinahusu..... zile Ngurumo saba zilizotoa sauti zao na hakuna yoyote angetambua ilikuwa nini..... Yohana alijua zilikuwa nini yeye alisema, “Lakini yule malaika wa saba katika siku za kupiga baragumu yake, zile siri saba za zile Ngurumo saba zitafunuliwa. “Na yule Malaika wa saba ndiye mjumbe wa saba wa ule wakati wa saba wa Kanisa.

Ni katika wakati wa mwisho ambapo ndipo zile Ngurumo Saba za Yesu zilipotoa sauti zao. Ufun.10:3-4

“Naye akalia kwa sauti kuu, kama Simba angurumavyo. Na alipolia, zile Ngurumo saba zikatoa sauti zao. Hata Ngurumo saba zilipotoa sauti zao nalikuwa tayari kuandika. Nami nalisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo Ngurumo saba, usiyaandike.” Kile kilichokuwa kwenye Ngurumo hizo hakuna ajuaye. Lakini tunahitaji kujua. Na itatakiwa nabii kupata ufunuo kwa maana Mungu hana njia nyingine ya kutoa mafunuo yake ya kimaandiko ila kwa njia ya nabii.

Neno daima linakuja kwa nabii na daima litamjia. Lakini alikatazwa asiandike, kwa hivyo tunaona malaika wa wakati wa saba akija, naye ni nabii. Si kwamba tu tunamwona mjumbe huyu akija hapa katika Ufu.10:7 lakini tunaona ya kwamba Neno linazumza juu ya Eliya akija kabla ya Yesu kurudi.

Tazama, Mungu alimwambia nabii akisema kula gombo katika agano la kale (Ezekiel3:1-3). Nabii wa agano JIPYA alisema “kula kitabu kidogo” Kwa nini? Kwamba Nabii na Neno walikuwa kitu kimoja. Unaona? Hilo sanduku la Bwana. Neno la Mungu.

Nukuu:

Watiwa mafuta wa nyakati za mwisho 25-7 ukurasa wa 23, para 91
-Kristo akifunuliwa katika Neno lake mwenyewe”22-08-65 para72-73
-Ufunuo kitabu cha mifano”17-06-56uk13-14 para64
-Laodikia wakati wa saba wa kanisa” uk 324
-Ufunuo sura4 sehemu ya 3,kiti cha enzi cha rehema na kiti cha enzi cha rehema na hukumu”8-1-61 para120
-Ufunuo sura ya 5 sehemu ya 2”18-06-61 para 100’207
-Hii ndiyo ishara ya mwisho Bwana”30-12-62 jioni uk,48
“ushawishi”-12-01-63 para 146
“Mungu katika urahisi”17-03-63 Asubuhi,uk,23 para 103
“pengo”17-03-63 jioni uk 78-80
“Muhuri wa kwanza”18-03-65 para 14,142; uk 128
“Muhuri wa pili” 19-03-63 para 351 uk
“Muhuri wa tatu”20-03-63 uk268 para 183,
“Muhuri wa saba” 24-03-63 jioni,uk 573;598;618; para 77;552;391
“Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa” para 105-108;205
“Mungu aliye funuliwa” uk 49 para273,
“Sikukuu ya baragumu”Uk 38-39 para 264-270(19-07-64)
“Maswali na majibu”30-08-64 jioni swali No. 395 C.O.D Uk wa 1047 para 78
“nyakati saba za kanisa wakati wa kanisa la Laodikia” Uk 320

“kujaribu kumfanyia Mungu kazi”27-11-65b para 319
-Jiwe lakujengea la kiroho No.116 kutoka kwenye eneo la wakati huu.....”

jiwe la kiroho la kujengea na 106 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@live1.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*